


Ufahamu Kutoka kwa **WAKULIMA**



Picha 1: Muonekano wa ukame
wa wastani katika kijiji cha Ilindii

Vipando Vinne Vya Viazi Lishe Marando ya Dhahabu (Kujenga uwezo wenyewe matokeo)


"Kwa sasa ninaweza
kupata kipato kutokana
na kuzalisha na kuuza
marando ya viazi lishe.
Kutokana na hilo
ninaweza sasa kulipa
ada ya shule kwa ajili ya
watoto wangu na pia
familia yetu ina chakula
cha kutosha na chenye
lishe"

Mkulima Julius Kayongola



Picha 2: Bwana Julius Kayongola, mkulima aliyepeata aina
4 ya vipando kutoka SRI – Kibaha kwa uzalishaji kuanzia,
Desemba 2015


Mashamba ya kuzalishia marando ya viazi lishe yaliyopo
katika kijiji cha Ilindi ni yenye kuvutia na kutia hamasa.
Mashamba hayo yanaangaliwa na wazalishaji wa viazi lishe
waliojitoa kwa nia moja na wanaotumia umwagiliaji kutoka
katika ziwa la karibu la Manyara. Ukaribu wa mashamba na
ziwa unafanya kina cha maji kiwe juu na hivyo kuwawezesha
wakulima kuchimba visima vya kumwagilia mazao yao.

Kijiji cha Ilindi kipo katika eneo lenye ukame wa wastani
katika Wilaya ya Bahi Mkoa wa Dodoma, Tanzania. Kutoka
barabara kuu huwezi kuona kitu chochote cha kijani wala
uzalishaji wowote; hadi utakapofika kwenye uoto wa ukijani
wa mashamba mazuri ya kuzalisha marando ya viazi lishe.

Bw. Julius Kayongola (katika picha kushoto) ambaye ni
mkulima wa kijiji cha Ilindi alisimulia safari aliopita hadi
kuwa mzalishaji wa kuaminika wa viazi lishe na marando yake.
Mwezi Desemba, 2015 mkulima huyu, alikuwa mmoja wa
wanufaika wa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu na marando
ya viazi lishe yaliyoandaliwa na Kituo cha Utafiti wa Sukari cha
Kibaha, Tanzania (SRI – Kibaha) kwa ufadhilli wa Shirika la
Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO).

Bwana Julius alielezea kuwa baada ya kupata mafunzo,
alipewa vipando vinne vya viazi lishe kwa ajili ya kuongeza
marando zaidi ambayo mpaka sasa ameshazalisha katika
shamba lenye ukubwa wa nusu (1/2) eka kwa kutumia
umwagiliaji. Vilevile aliwagawia marando ndugu wa familia na
majirani na kwa kitendo hicho wanajamii wengi wa kijiji cha
Ilindi sasa wanazalisha na kula viazi lishe mwaka mzima.
Wakulima wa viazi lishe wanazalisha aina kadhaa za marando
ya viazi lishe na kuyauza katika masoko yaliyopo maeneo yao
na hivyo kujiongezea kipato.

Viazi lishe aina ya "Ejumula" ni moja ya aina inayopendwa sana
na wakulima wa Kijiji cha Ilindi. Aina hii inakua vizuri katika
hali ya ukame wa wastani na inazaa viazi vikubwa (angalia
picha 4). Viazi hivi hukamilisha mlo wenyewe lishe ambao
unaliwa na wanajamii wengi katika kijiji cha Ilindi.



CIP
INTERNATIONAL POTATO CENTER
A CGIAR RESEARCH CENTER



CIAT
International Center for Tropical Agriculture
Since 1969 / Science to cultivate change

CIMMYT
International Maize and Wheat Improvement Center



IITA
Research to Nourish Africa



HarvestPlus
Better Crops - Better Nutrition



FARA
Forum for Agricultural Research in Africa





Picha 3: Shamba la nusu eka la uzalishaji wa viazi lishe la mkulima Julius Kayongola

Maelezo na simulizi ya Bw. Julius ni mfano mzuri wa matokeo chanya na uendelezaji wa mradi wa kuleta mabadiliko (RAC) kutokana na juhudzi za kujenga uwezo kwa walengwa. Katika mwaka 2011 na 2014, Kituo cha Kimataifa cha Viazi (CIP) na Taasisi ya Kimataifa ya Helen Keller (HKI) walitekeleza mradi wa kuleta mabadiliko (RAC), ambao ulikuwa unalenga kuongeza uwekezaji katika viazi lishe ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa vitamini A kwa watoto wadogo na wanawake walio katika umri wa uzazi. Mradi wa RAC ulijenjea uwezo wadau wa kitaifa kama vile Kituo cha Utafiti wa Sukari Kibaha (SRI- Kibaha), Tanzania na wanufaika wengine



Picha 4: Aina ya viazi lishe vinavyoimwa kijiji cha llindi

muhimu ili kuwawezesha kujipanga, kuwa na malengo, kupokea mradi, na kupeleka ujuzi walioupati kwa wanufaika wengine wa chini zaidi kama vile wakulima.

Katika kutekeleza mradi huu, mwaka 2015 kituo cha utafiti cha SRI – Kibaha kilipokea msaada wa dola za Marekani 20,000 kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO). Hayo yalikuwa moja ya matokeo ya juhudzi zilizofanywa na RAC ambapo zaidi ya dola za marekani 21.6 milioni zilipatikana kwa ajili ya mipango ya uzalishaji viazi lishe na uboreshaji wa lishe kujitia matumizi ya vyakula katika nchi zilizolengwa kutekeleza mradi za Nigeria, Tanzania, Musumbiji, Ghana na Burkina Faso. Vituo vya utafiti wa Kilimo vya SRI – Kibaha na ARI – Hombolo, ni baadhi ya taasisi ambazo zilijengewa uwezo na RAC katika kutoa mafunzo kwa wawezeshaji (ToTs) ya "kila unachotaka kufahamu kuhusu viazi lishe". Kwa sasa wanaendeleza ujuzi na utaalalm kwa maafisa ugani, wakulima na wadau wengine juu ya mnyonyoro wa thamani wa viazi lishe ili kuhakikisha kuwa matokeo chanya yanaifikia jamii yote.

Vituo vya utafiti vya SRI – Kibaha na ARI – Hombolo viliweza kutumia mafanikio aliyoypata Bwana Julius katika kuwawezesha na kuwatia hamasa wakulima

wengine wa viazi lishe kujitia mafunzo ya kutembeleana kwenye mashamba ambayo ilikuwa ni sehemu ya mafunzo ya siku 2 juu ya kilimo na uzalishaji wa mbegu za viazi lishe yaliyofanyika tarehe 26 – 27 Septemba, 2016.

Mafunzo yaliwalenga maafisa ugani na wazalishaji wa marando ya viazi lishe kutoka katika wilaya 6 za mkoa wa Singida na wilaya 6 za Mkoa wa Dodoma. Lengo la mafunzo hayo ilikuwa kuwapatia washiriki elimu, ujuzi, utaalalm na uelewa wa kuzalisha mbegu za viazi lishe.

Uzinduzi wa mpango wa miaka 4 wa Kilimo cha viazi lishe katika kijiji cha llindi

Hatimaye, katika siku za karibuni kijiji cha llindi kilizindua mpango wa miaka 4 wa kuzalisha viazi lishe utakaohakikisha kuwa kaya zote 22,000 zinalima na kula viazi lishe kufikia mwaka 2020. Mpango huu unalenga kuongeza uhakika wa chakula na lishe kwa ajili ya jamii ya llindi na kuongeza kipato katika familia.

Mradi huu wa viazi lishe (OFSP) unasimamiwa na Bwana Anthony Sahali, Afisa Ugani wa Kata kwa kushirikiana na watu wengine mashuhuri wa viazi lishe akiwemo Bi. Tina Suday Mbassa ambaye pia ni Diwani wa Kata.

Mafanikio yaliyopatikana pamoja na malengo yaliyofikiwa na mambo mengine waliyofunza kutoka kwenye mradi wa RAC yaliwezesha kuanzishwa kwa mradi mwingine wa

Kuimarisha Lishe ya Makundi ya Vyakula Mchanganyiko (Building Nutritious Food Baskets – BNFB). Mradi huu wa



Picha 5: Jamii ya llindi ikizindua mpango wa miaka 4 wa viazi lishe

BNFB unalenga kuangalia uwezekano wa kupanua mfumo wa utekelezaji kujitia utaratibu wa vyakula mchanganyiko katika kukabiliana na njaa iliyojificha ya upungufu wa virutubishi vya vitamini na madini kwa kuhimiza uwezekaji endelevu katika kuongeza uzalishaji na matumizi ya mazao yaliyorubishwa kibailolojia kama vile viazi lishe, mihogo lishe (mihongo manjano), mahindi lishe (mahindi ya chungwa), na maharage lishe (yenye wingi wa madini chuma au zinki).

Miradi ya RAC na BNFB inafadhiliwa na kusaidiwa na Mfuko wa Bill & Melinda Gates Foundation

Jifunze zaidi kuhusu Kuimarisha Lishe ya Makundi ya Vyakula Mchanganyiko (Building Nutritious Food Baskets – BNFB)

Bofya Building Nutritious Food Baskets (BNFB)